AngloGoldAshanti

Sheria ya Maadili na Kanuni za Biashara

SWAHILI VERSION

MAADILI YETU

Usalama
Tunaupa usalama kipaumbele, kabla ya kitu kingine chochote

Heshima
Tunahusiana baina yetu kwa utu and heshima

Uwajibikaji
Tunajitahidi kutimiza ahadi zetu kwa ukweli na uaminifu

Uendelevu
Tunachangia kwa njia chanya kuhakikisha kuna mazingira safi ya kudumu duniani

Ubora
Tunazingatia kufanya uboreshaji mfululizo ili kuimarisha utamaduni wa utendaji wa hali ya juu

Ushirikiano
Tunafanya kazi pamoja kujenga kampuni bora zaidi

Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu

AngloGold Ashanti ina historia ndefu, ya kujivunia kama shirika linaloendeshwa kwa kuzingatia kanuni na maadili.

Kwa muda mrefu tumelenga kufanya jambo sahihi kila wakati kama msingi wa jinsi tunavyofanya biashara, na ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba tunaendelea kufuata msimamo huu.

Maadili Yetu yanaeleza kuhusu tabia muhimu katika kujenga biashara ya madini yenye mafanikio, uendelevu na faida kwa muda mrefu. Maadili haya, yaliyojengwa kwa kuchukua maoni kutoka kote ulimwenguni, yanatuagiza kuweka usalama kuwa kipaumbele kikuu zaidi; kumtendea kila mtu tunayekutana naye kwa utu na heshima; kudumisha viwango vya juu vya uaminifu na uadilifu; kuchangia kwa njia chanya kwenye mazingira yetu na jamii za wenyeji; na kuthamini sana ushirikiano tunapojenga utamaduni wa ubora.

Sheria yetu ya Maadili hutusaidia kutekeleza Maadili haya kwa kufafanua tabia ambayo kila mtu anayefanya kazi katika biashara yetu anatarajiwa kuonyesha, kuanzia kwa wakurugenzi na viongozi wetu hadi wakandarasi na washauri, na kila mtu aliye katika viwango hivi viwili. Pia inaeleza hatua rahisi ambazo kila mmoja wetu amewezeshwa kuchukua, tunaposhuhudia tabia ambayo haiendani na Kanuni Zetu.

Sheria zetu ni Dira inayoelekeza vitendo na tabia ambazo zitahakikisha mafanikio ya muda mrefu ya AngloGold Ashanti, kwa namna ambayo sote tunaweza kujivunia.

Kwa dhati,
Alberto Calderon
Afisa Mtendaji Mkuu

Alberto Calderon
Afisa Mtendaji Mkuu
AngloGold Ashanti

Utangulizi

Sheria ya Maadili na Kanuni za Biashara (Sheria) ni muhimu kwa utamaduni wetu wa utendaji na uadilifu.

Sheria hii inaelezea matarajio yetu kuhusu mienendo ya wakurugenzi wetu, wafanyakazi, makandarasi na washauri, na inasisitiza dhamira yetu ya kufuata viwango vya juu kabisa vya uadilifu na maadili katika uendeshaji biashara yetu.

Tunachukulia maadili yetu kuwa msingi wa kukuza mahusiano yaliyojengwa kwa msingi wa uaminifu wa wahusika wote, na kama njia ya kutusaidia kuchangia mafanikio ya pamoja ya kampuni yetu. Sisi sote tuna jukumu la kudumisha maadili na kanuni zinazohimiza jinsi tunavyofanya kazi – usalama, heshima, ubora, ushirikiano, uadilifu na endelevu. Kanuni hizi lazima zitumike kuongoza tabia yetu ndani ya kampuni na pia katika mahusiano yetu na washirika wa biashara na ndani ya jamii ambapo tunafanya kazi.

Ni jukumu la kila mmoja wetu kusoma, kuelewa na kutii viwango vilivyomo katika Sheria hii, kujenga uhusiano wa ndani na nje unaotokana na uadilifu na heshima, na kuepuka shughuli ambazo zinaweza kuathiri sifa za kampuni hii.

Sheria hii inawakilisha matarajio ya AngloGold Ashanti na haijaandaliwa kwa lengo la kushughulikia hali zote zinazowezekana ambazo zinaweza kutokea. Unatarajiwa kutazama Sheria hii kama mwongozo na marejeleo ya kutekeleza maadili yetu.

Kila mkurugenzi, mfanyakazi, mkandarasi na mshauri ana jukumu la kutii Sheria hii, sera, viwango na taratibu za AngloGold Ashanti na sheria, kanuni na viwango vyote vinavyohusiana na biashara yetu na shughuli zetu katika nchi zote ambapo tunafhudumu, pamoja na masharti mengine ambayo tumejitolea kuzingatia. Marejeo yoyote kuhusu AngloGold Ashanti yanajumuisha kampuni zake tanzu na washirika wake, ikiwa ni pamoja na migodi yoyote binafsi inayowekwa katika mikataba na wauzaji kwa majina yao wenyewe.

Kuvunja Sheria hii kunaweza kusababisha hatua za kinidhamu (ikiwa ni pamoja na kufutwa kazi). Wakati mwingine, tabia ambayo inakiuka Sheria hii inaweza pia kuwa uvunjaji wa sheria na kusababisha adhabu za kiraia au mashtaka ya jinai

Kanuni

Tunaweka usalama mbele, kabla ya kitu kinginecho.

Tunawaweka watu mbele na kutanguliza utendakazi salama na mifumo ya kazi. Tunahakikisha kudumisha afya ya watu na kuwalinda dhidi ya athari za kiafya, kiakili au kihisia zinazoweza kuhatarisha ustawi wao kazini.

Kuweka kipaumbele cha afya na usalama ni jitihada za pamoja. Kila mmoja wetu ana jukumu binafsi na la pamoja la kuwajibikia afya, usalama na ulinzi wetu na wa wengine, kushiriki mambo tunayopitia na kujifunza kutoka kwa kila mmoja.

Tunatendeana kwa heshima na utu.

Tunamtendea kila mtu kwa heshima na tunajitahidi kudumisha heshima na utu wa kila mtu katika mahusiano yetu yote, tukiheshimu wengine kwa utu wao, na kuthamini mchango wa kipekee ambao wanaweza kutoa katika mafanikio ya biashara yetu.

Tunathamini na kuwaunga mkono watu wetu na tumejitolea kukuza na kudumisha mazingira ya kazi yenye uwazi inayopokea na kujivunia utofauti na usawa. Tumepiga marufuku aina zote za unyanyasaji, vurugu, udhalilishaji, udhalilishaji wa kijinsia na ubaguzi, na tumejitolea kudumisha mazingira ya kazi ambapo kila mtu anatendewa kwa haki na heshima.

Tunaheshimu haki za binadamu za wadau wetu wote, ikiwa ni pamoja na haki za watu wa kiasili na makundi yaliyohatarishwa, na tunaheshimu maadili, mila na tamaduni za jamii za wenyeji na za Kiasili ambapo tunafanyia kazi.

Tunafanya shughuli zetu za biashara kwa uaminifu.

Tunajitahidi daima kufanya kazi kwa lengo la kulinda maslahi ya AngloGold Ashanti na kuhakikisha kuwa watu wetu wanatekeleza majukumu yao kwa uaminifu na uwazi. Tunatimiza ahadi hii kwa kufuata sheria, viwango na kanuni zote husika, na kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na udanganyifu, rushwa na mienendo mbaya husika.

Tunakwepa hali ambapo maslahi ya AngloGold Ashanti na maslahi yetu binafsi yanagongana au yanaonekana kugongana, na hatutakiwi kukubali zawadi au vitendo vya ukarimu ambavyo vinaweza kuathiri maamuzi sahihi kutoka kwetu. Tunafanya shughuli zetu za biashara kwa uaminifu na tunapigania ushindani wa haki sokoni. Tunawahimiza watu wetu kutoa maoni iwapo watatambua tabia zozote ambazo haziendani na maadili na kanuni za biashara za AngloGold Ashanti.

Kanuni continued

Tunatoa michango chanya ili kujenga dunia bora ya kudumu.

Tumejitolea kuhakikisha kuwa jamii na jumuiya ambapo tunafanyia kazi zinafaidika kutokana na uwepo wa AngloGold Ashanti. Tunakuza ushirikiano, uliojengwa kwa msingi wa kuheshimiana na kuaminina, katika jamii ambapo tunafanyia kazi. Tunachangia katika maendeleo ya kudumu kwa kuheshimu na kukuza haki za binadamu za washikadau wetu wote katika jamii ambapo tunafanyia kazi.

Tunajitahidi kupata matokeo endelevu kwa kusimamia kwa uwajibikaji rasilimali asili ambazo sisi ni watunzaji wake, na kupunguza uwezekano wa kuharibu mazingira kutokana na shughuli zetu. Tunashauri kuwa na mtazamo wa tahadhari kuhusiana na changamoto za mazingira, kuanzisha mpango ya kukuza uwajibikaji mkubwa zaidi wa kimazingira, kuchochea maendeleo na usambazaji wa teknolojia zinazolinda mazingira, na lengo letu ni kupunguza viwango vyetu vya kuathiri mazingira.

Tunazingatia uboreshaji endelevu ili kujenga utamaduni wenye ufanisi wa hali ya juu.

Tunalenga kupata matokeo bora na tunatimiza ahadi tunazotoa. Tunakubali jukumu na tunawajibikia kazi yetu, tabia zetu, maadili yetu na vitendo vyetu.

Tunalenga kupata matokeo bora ya utendaji na tunaahidi kutimiza ahadi tulizowapa wenzetu, biashara, washirika wa kijamii, na wawekezaji wetu. Tunahamasisha na kuchukua fursa za kukua kitaalamu na kibinafsi, na daima tunatafuta mbinu za kuboresha mambo.

Pia tunajitolea kulinda usalama na thamani ya rasilimali zetu ikiwa ni pamoja na fedha, miundombinu, mali isiyohamishika, mali ya kiakili, rasilimali za kielektroniki na miundombinu ya habari.

Tunashirikiana kujenga kampuni bora zaidi.

Tunatambua kuwa kukuza na kudumisha mazingira ya kazini yanayomjumuisha kila mtu na kujivunia tofauti kutaimarisha uwezo wetu wa kushirikiana, kubuni na kupata matokeo bora katika biashara yetu.

Tumejitolea kushirikiana na watu wetu ili kuhakikisha tunao watu sahihi, tumewapa majukumu sahihi, wakati sahihi na wanaweza kukuza uwezo wao kikamilifu. Tunathamini na kuzingatia utaalamu wa kila mmoja wetu na tunawaleta watu pamoja kutathmini fursa na kutatua matatizo.

Rasilimali na nyenzo nyinginezo muhimu

Sheria hii inaakisi maadili ya kampuni na ni chanzo cha maelekezo na mwongozo ya matendo na maamuzi yetu ya ndani ya kampuni, na katika uhusiano wetu na washikadau wetu wote.

Kanuni hii inatoa mfumo na kuweka masharti ya chini zaidi ya utekelezaji wa sera, maadili na kanuni zetu.

Mfumo wetu wa utawala wa ndani unajumuisha Sera za Kampuni nzima zilizoorodheshwa hapa chini, pamoja na Viwango, Taratibu na nyaraka nyingine muhimu (zinapatikana kwenye https://www.anglogoldashanti.com/sustainability/governance/policies-standards/). Wafanyakazi wa AngloGold Ashanti wanaweza kupata nakala za kielektroniki za nyaraka zote kwenye mtandao wa ndani wa kampuni.

- ***Sera ya Usalama wa Rasilimali na Ulinzi wa Maadili***
- ***Sera ya Uadilifu wa Kibiashara***
- ***Sera ya Afya, Usalama na Ulinzi***
- ***Sera ya Utendakazi na Ukuzaji Rasilimali za Madini***
- ***Sera kuhusu Watu***
- ***Kanuni ya Maadili ya Wauzaji***
- ***Sera ya Uendelevu***

Ikiwa una maswali kuhusu Sheria yetu, unaweza kuwasiliana na meneja au msimamizi wako, mwanachama wa kitengo cha Kutii Sheria cha Kampuni au kitengo cha Sheria cha Kampuni, au unaweza kuwasilisha wasiwasi wako kupitia mbinu za ufichuzi za AngloGold Ashanti. Tafadhali rejelea Sera za Ufichuzi upate maelezo zaidi kuhusu mada hii.

Speak-up

Kwa sababu ni jambo jema kulifanya

Kimataifa Tel. +27 31 571 5654
Email: SpeakupAGA@ethics-line.com
Piga simu utendaji +27 11 929 3332 - See Intranet
Fax: +27 31 560 7395
Post: PO Box 774, Umhlanga Rocks, 4230, South Africa.
Tovuti: https://www.tip-offs.com
Tuma ujumbe “Speak-up” kwenda ili kupokea ujumbewa maelekezo +27 73 573 8075
(viwango vya huduma za simu vya kimataifa vitatumika)

Shukrani

Nimeisoma Sheria hii, au, ikiwa sijaisoma, ninakubali jukumu la kujifahamisha kuhusu yaliyomo.

Nitatii Sheri ahii, pamoja na Sera, Viwango, Taratibu, Miongozo na taarifa zingine husika ambazo zinaweza kutumika kudhibiti kazi yangu kwa kampuni. Ninaelewa kwamba ninaweza kujadiliana na msimamizi wangu kuhusu maswali au wasiwasi wowote nilio nao kuhusu Kanuni au Sera, Viwango, Taratibu, Miongozo na taarifa zingine zinazofanana na hizo ambazo zinaweza kutumika kudhibiti kazi yangu katika kampuni hii. Maswali yoyote niliyokuwa nayo kuhusu Kanuni; Sera, Viwango, Taratibu, Miongozo na taarifa zingine husika; na/au Shukrani hii yalijibiwa hadi nikaridhika kabla ya kuweka saini kwenye Shukrani hii.